



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE



Tarehe: 17/07/2023

TANGAZO LA AJIRA YA MKATABA KWA AJILI YA UJENZI WA NYUMBA YA
MKURUGENZI

ZABUNI NA: LGA/071/2023/2024/RDC/W/05

1. **Mkurugenzi Mtendaji (W)** anawatangazia Wananchi wote kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe imepokea fedha kwa ajili ya ujenzi wa **Nyumba ya Mkurugenzi Mtendaji** katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kupitia Fedha za **Miradi ya Maendeleo kutoka Serikali Kuu** kwa mwaka wa fedha 2023/2024.
2. Hivyo basi, Mkurugenzi Mtendaji (W) anakaribisha Mafundi ujenzi wenye sifa na uzoefu katika shughuli za ujenzi wa Miundo mbinu ya Serikali kuomba kazi za Ufundi kwa utaratibu wa **"Force Account"** katika fani na sifa za Ufundi zifuatazo:-
 - i. **Fundi Uashi** (ambao utajumuisha na upakaji wa rangi, Ufungaji wa Mifumo ya maji safi na Maji taka na Ufundi umeme),
 - Awe na elimu ya ufundi ujenzi (Angalau Diploma/FTC na mwenye kujua vyema kusoma ramani za majengo na kutafsiri).
 - Awe na vitendea kazi za kunyoosha ukuta kama vile Square, bridge (Plumb Bob), mwiko, Komabao, Pima maji n.k
 - Awe amewahi kufanya kazi ya ujenzi katika majengo ya Serikali au kwenye makampuni.
 - ii. **Fundi Aluminium**
 - Awe na uwezo wa kusoma michoro na vipimo vya ramani.
 - Awe na uwezo wa kutengeneza madirisha ya Aluminium na milango ya alco bond).
 - Awe amewahi kufanya kazi ya ujenzi katika majengo ya Serikali au kwenye makampuni.
 - iii. **Fundi Seremala** (inahusisha utengenezaji wa milango na fremu za milango).
 - Awe na uwezo wa kutengeneza milango ya mbao ngumu
 - Awe amewahi kufanya kazi ya ujenzi katika majengo ya Serikali au kwenye makampuni.

- iv. **Fundi kuchomelea vyuma** (ambao utajumuisha kutengeneza magrill ya milango, madirisha na baluster/Hand rail) na bembea za watoto.
- Awe na uwezo wa kutengeneza milango ya "grill", baluster na madirisha
 - Awe amewahi kufanya kazi ya ujenzi katika majengo ya Serikali au kwenye makampuni.

3. **Pamoja na sifa zilizotolewa hapo juu waombaji wanapaswa kuzingatia masharti kama ifuatavyo:-**

- Awe Mtanzania mwenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea
 - Awe na Namba ya Utambulisho wa mlipa kodi (TIN) (aambatanishe na barua ya maombi kwa uthibitisho zaidi)
 - Awe na akaunti ya benki kwenye benki yeyote iliyopo ndani ya Rungwe.
 - Mwombaji aambatanishe barua ya utambulisho kutoka ofisi ya Afisa Mtendaji wa Kijiji/Kitongoji/Mtaa anakoishi.
 - Awe tayari kufanya kazi muda wote hadi mradi utakapokamilika
4. Barua za maombi zikiwa zimeambatanishwa na nyaraka tajwa hapo juu ziwasilishwe ofisi ya Mwalimu Mkuu, **Shule ya Sekondari Msasani One, S.L.P 148, Tukuyu** yakiwa yamefungwa kwenye bahasha nyuma ya bahasha ikitaja jina la kazi ya Ufundi unaoombwa mfano **Ufundi Uashi au Seremala n.k**
5. Mwisho wa kupokea maombi ya kazi za ufundi ni siku ya Ijumaa ya Tarehe 24/05/2023 kabla ya saa 5:00 Asubuhi. Aidha, maombi yatakayoletwa baada ya hapo hayatakubaliwa.
6. Waombaji wote wanatakiwa kuhudhuria usaili wa mafundi wa utakaofanyika tarehe 24/05/2023 saa 5:30 Asubuhi utakaombatana na kuwashindanisha nukuu za bei za ufundi.
7. Wako katika ujenzi wa Taifa.



Mchau, R.B

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
RUNGWE